


Changanya mbegu mkono moja na fatalaiza aina ya superphosphate mikono miwili.



Ikiwa huwezi kununua fatalaiza basi changanya mbegu na udongo nyororo. Panda ndani ya mitaro na ufunike kwa udongo.



Palilia baada ya wiki sita.

Endelea kupunguza matawi ili isimee kati ya mimea ya mahindi.



Shamba lionekane hivi wakati mimea imekomaa.

Wakati gani na jinsi gani tunavuna mbegu za desmodium?

Vuna mbegu kila wiki pindi maganda yakiwa rangi ya kahawia (Brown). Chuma maganda kwa mkono na uziweke mbegu ndani ya mkebe.



Kausha mbegu kwa jua kisha twanga kwa jiwe.



Pepeta mbegu ili uondoe uchafu wote.



Hifadhi mbegu zako ndani ya debe au ndani ya chombo kisicho ruhusu hewa kuingia katika mahali pakavu.

Mbegu za Desmodium ina bei mzuri kwa hivyo, uza mbegu zako sokoni

Produced by Mediae Trust
PO Box 39486 Nairobi. Tel 442660

Kuza Desmodium na Uzuie Kwekwe la Striga



Panda desmodium pamoja na mahindi ili izuie kwekwe la Striga kukuwa ndani ya shamba lako la mahindi

Wadhamini:

Gatsby Charitable Foundation,
ICIPE, IACR- Rothamsted,
KARI na Wizara ya Kilimo, Kenya

Je, umewahi kuliona kwekwe hili ndani ya shamba lako la mahindi

Kwekwe lenyewe linaitwa striga.



Striga linaweza kuadhiri mazao yako namna gani?

Striga inaweza kusababisha upotevu wa nusu ya mimea yako. Ikiwa hapo awali ulikuwa unavuna magunia kumi ya mahindi lakini striga ikivamia shamba lako utavuna magunia matano tu.

Kwekwe la striga linaadhiri shamba lako namna gani?

Kwekwe la striga linaingiza mizizi yake ndani ya mizizi ya mahindi au mtama.



Kwekwe linapokonya chakula cha mahindi kutoka ndani ya udongo kabla hakijafikia mmea ya mahindi.

Tunawezaje kuzuia striga?

Njia nyingi zilizopendekezwa hazifanyi kazi.

- Ng'oa kwekwe la striga na uhome nje ya shamba.
 - Hii ni kazi nyingi na ngumu lakini baadaye striga inarudi.
- Tumia dawa ya kuua makwekwe.
 - Njia hii ina gharimu pesa nyingi lakini baada ya muda makwekwe yanarejea tena.
- Panda aina za mahindi zinazovumilia striga.
 - Makwekwe hayajapotea, njia hii ina kazi nyingi na mazao kila mara ni machache.
- Tia fatalaiza nyingi ili mahindi yatoe mazao mengi hata kama kuna striga.
 - Mbinu hii inagharimu pesa nyingi, kazi ni nyingi na makwekwe hayajaenda.

HABARI NJEMA

Ni mbinu gani inayoweza kufanya kazi?

Imegunduliwa kuwa ukipanda desmodium pamoja na mahindi unazuia striga kumea katika shamba la mahindi.



Mbinu hii inafanya kazi namna gani?

Mmea wa desmodium unafunika udongo wote kati ya mistari ya mahindi. Desmodium inatia aina ya kemikali isiyopendelewa na striga ndani ya udongo. Kwa hivyo, striga haitamea kule desmodium inakuzwa

Kwa nini desmodium ni mmea mzuri?

- Inazuia striga kumea.
- Inarudisha nitrogen ndani ya udongo.
- Ni malisho bora kwa ng'ombe wa maziwa.
- Inafunika udongo wote, kwa hivyo, inazuia maji kupotea na inazuia mmomonyoko wa udongo.
- Baadhi ya wakulima watanunua mbegu zako za desmodium kwa bei mzuri.

Mazao yataongezeka kwa kiwango gani?

Ikiwa unavuna magunia kumi ya mahindi ukiwa na striga shambani bila striga utavuna hadi magunia kumi na tano ya mahindi na utakuwa na majani mabichi kwa mwaka mzima kwa ng'ombe wako wa maziwa.

Tunakuzaje desmodium pamoja na mahindi?

Upate mbegu za desmodium kutoka-

- Kenya Seed Company
- ICIPE, Mbita Point, Suba District
- Jirani wako aliyeanza kukuza desmodium.

Utahitaji karibu kilo moja kwa kila ekari.

Tayarisha udongo kwa uangalifu na ulainishe barabara.

Chimba mitaro katikati ya mistari ya mahindi. Tumia kijiti kilichochongwa.

